

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Zanzibar

13 Februari, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali na kumpangia kituo cha kazi Balozi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, uteuzi na kupangiwa kituo ni kama ifuatavyo:-

- i. Dkt. Amina Suleiman Msengwa ameteuliwa kuwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu, Dkt. Msengwa alikuwa Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dkt. Msengwa anachukua nafasi ya Dkt. Albina Chuwa ambaye amemaliza muda wake;
- ii. Jaji Dkt. Ntemi Nimilwa Kilekamajenga ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Masoko na Mitaji. Jaji Dkt. Kilekamajenga anachukua nafasi ya Jaji Dkt. Deo John Nangela ambaye aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani;
- iii. Prof. Aurelia Kamuzora ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Kahawa. Prof. Kamuzora ameteuliwa kwa kipindi cha pili;
- iv. Bw. Abdulmajid Nsekela ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Chai Tanzania. Bw. Nsekela anachukua nafasi ya Bw. Mustafa Hamis Umande ambaye amemaliza muda wake;
- v. Prof. Hozen Kahesi Mayaya ameteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP). Prof. Hozen ameteuliwa kwa kipindi cha pili; na
- vi. Balozi Dkt. Habib Galuss Kambanga amepangiwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Rwanda.

Sharifa B. Nyanga

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano /
ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania /
ikulumawasiliano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania

